

102/3

KISWAHILI

KARATASI 3

(INSHA)

JULY/AUGUST – 2009

MUDA:Saa 1 ¾

MTIHANI WA MWIGO WA INTERZONAL

HATI ya kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenaya.

Maagizo

Jibu maswali manne tu.

1. Fasihi simulizi
 - (i) Methali ni nini? (alama 2)
 - (ii) Eleza tofauti baina ya methali na misimu katika fasihi simulizi (alama 8)
 - (iii) Methali zina umuhimu gani katika jamii? (alama 10)

2. TAMTHILIA Kifo Kisimani

Taja na ufafanue sifa za:

- (i) Mwelusi
- (ii) Bokono (alama 20)

3.RIWAYA: Utengano

- a) Taja na ufafanue aina za utengano katika riwaya ya utengano (alama 10)
- b) Eleza vile maudhui yafuatayo yamejitokeza katika Utengano (alama 10)
 - (i) Uozo wa jamii
 - (ii) Ubinafsi
 - (iii) Taasubi ya kiume
 - (iv) Ufisadi
 - (v) Sheria
- 4 hadithi fupi – Mayai Waziri wa Maradhi
Fafanua matatizo yanayozikumba nchi nyingi za ulimwengu
wa tatu ukirejelea hadithi ya Mayai waziri wa Maradhi (alama 20)

5.(USHAIRI)

Soma shairi hil kasha ujibu maswali

1. Wasiwasi n'ondokeya, ondoka enenda zako
Ondoka andama ndiya,n'ondosheya uso wako

- Ondoka! Wanisikiya?Ziwate jeuri zako.
Jishughulishe na yako, yangu wayatakiyani?
2. Wasiwasi sitaki, suhuba yako si nzuri
Haisitahamiliki, uwove umekithiri
Inganyoshwa hainyoki, ikukutene kikiri
Sitaki yako shari, enda zako wasiwasi
 3. Huna kazi ufanyayo, ela kuwafitinisha
Viumbe na zao nyoyo, vitwa kuwagotanisha
Hiino ndiyo kaziyo, yenye kukufurahisha.
Ni kazi isokuchosha, mno umizoweya.
 4. Tukaapo wanmbiya, hayawi niyatakayo
Kwamba tama ngatiya, nasumbuwa wangu moyo
Kwamba hata hingojeya, hayo niyangojeyayo
Ng'o! siyapati hayo, ni bure najisumbuwa
 5. Mara waja na habari, mambo yalivyo nyumbani
Ati mambo si mazuri, mambo yote tafashani
Wanitaka nifikiri, usemayo ni yakini
Nisononeke moyoni, upate kufurahika.
 6. Au mara hunijiya, na kingine kisahani
Kuhusu zao afiya, hao waliyo nyumbani
Huwa hwishi kunambiya, hali zao taabani
Zingawa; watakiyani? Ni zako au ni zao?
 7. Na mara huja nambiya, nitakapotoka humu
Ya kwamba yaningojeya, nde maisha magumu
Ulilokusudiya, ni kunitiya wazimu?
Kama ndiyo yako hamu, basi ushatahayari.
 8. Hu urafiki wako, wa kuja niumngulisha
Kunipa masikutiko, na mateso yasokwisha
Kutoka leo ni mwiko, sitauktaka maisha
Kamwe hutanikondesha, tokomeya mwana kwenda.
- a) Eleza dhamira ya mwandishi katika shairi hili (alama 2)
 - b) Kwa kutolea mifano mwafaka, onysah jinsi mwandishi
alivyotumia uhuru wa shairi (alama 4)
 - c) Taja, ufafanue na kutolea mifano mbinu zozote mbili za lugha
katika shairi hili (alama 4)
 - d) Eleza muundo wa shairi hili (alama 4)

e) Andika ubeti wa nane katika lugha nathari (alama 2)

f) Andika maneno haya kwa Kiswahili sanifu.

i) ziwate

ii) Vitwa

iii) ndiya

iv) Nde